



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO**



**TANGAZO TANGAZO TANGAZO**

**MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA ANATARAJIA KUTOA MIKOPO INAYOTOKANA NA ASILIMIA 10 YA MAPATO YA NDANI KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.**

**VIKUNDI VYENYE SIFA ZILIZOAMBATANA NA TANGAZO HILI VIWASILISHE FOMU ZA MAOMBI YALIYOPITISHWA NA MTENDAJI WA KIJJI NA KATA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO KUANZIA TAREHE 03/01/2025 MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 31/01/2025.**

**VIKUNDI VIIBUE MIRADI MIKUBWA YENYE TIJA NA ENDELEU KWA MAENDELEO YA JAMII YA CHAMWINO.**

**TAFADHALI ZINGATI MUDA ULIOPANGWA**

**UONAPO TANGAZO HILI MJULISHE MWENZAKO**

**TANGAZO LIMETOLEWA LEO TAREHE 03/01/2022.**

**GODFREY MNYAMALE**

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W) CHAMWINO**

## SIFA ZA VIKUNDI

### KIKUNDI CHA WANAWAKE

- i. Kiwe cha wanawake kuanzia watano na kuendelea
- ii. Wanavikundi wawe na vitambulisho vya Taifa (NIDA) kila mmoja
- iii. Kiwe kimesajiliwa
- iv. Kiwe kinafanya shughuli za pamoja ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino
- v. Kiwe na akaunti inayotumika benki kwa jina la kikundi
- vi. Kisiwe na watumishi wenye ajira rasmi
- vii. Kisiwe na deni la mkopo

### KIKUNDI CHA VIJANA

- i. Kiwe cha vijana wa (wakiume/wakike/wakiume na wakike) kuanzia watano nakuendelea wenye umri kati ya miaka 18 hadi 45
- ii. Wanavikundi wawe na vitambulisho vya Taifa (NIDA) kila mmoja
- iii. Kiwe kimesajiliwa
- iv. Kiwe kinafanya shughuli za pamoja ndani ya Halmashauri Ya Wilaya ya Chamwino
- v. Kiwe na akaunti inayotumika benki kwa jina la kikundi
- vi. Kisiwe na watumishi wenye ajira rasmi
- vii. Kisiwe na deni la mkopo

### KIKUNDI CHA WATU WENYE ULEMAVU

- i. Kiwe cha watu wenye ulemavu kuanzia wawili na kuendelea (wawakilishi hawaruhusiwi)
- ii. Wanavikundi wawe na vitambulisho vya Taifa (NIDA) kila mmoja
- iii. Kisiwe cha watu wenye ulemavu wa akili
- iv. Kiwe kimesajiliwa
- v. Kiwe kinafanya shughuli za pamoja ndani ya Halmashauri Ya Wilaya ya Chamwino
- vi. Kiwe na akaunti inayotumika benki kwa jina la kikundi
- vii. Kisiwe na watumishi wenye ajira rasmi
- viii. Kisiwe na deni la mkopo